HALMASHAURI YA WILAYA YA

RUFIJI

MPANGO WA USIMAMIZI WA MISITU

YA TAWI

MPANGO WA USIMAMIZI IMEANDALIWA NA

SERIKALI YA KIJIJI CHA

TAWI

ULIOANDALIWA NOVEMBA 2006.

NA KUFANYIWA MABADILIKO

SEPTEMBA 2009

YALIYOMO

1: UTANGULIZI 3

1.1 Umiliki wa msitu 3
1.2 Lengo kuu la ya Mpango Shirikishi 3
1.3 Madhumuni 4
1.4 Muda 4

2: HISTORIA FUPI YA MPANGO 5

2.1 Jamii 5
2.2 Maelezo kuhusu Msitu 5
2.2.1 Mahali ulipo Msitu na ukubwa wake 5
2.2.2 Uoto wa asili na Mazingira. 5
2.2.3 Rasilimali za misitu. 5
2.2.4 Wanyama pori na jamii za mimea 6
2.3 Matumizi ya Msitu 7
2.3.1 Mambo ya asili & Haki za kijadi 7
2.3.2 Historia ya nyuma 7
2.3.3 Matumizi ya sasa 7

3: MWONGOZO WA MATUMIZI YA MAZAO YA MISITU. 8

3.1 Matumizi ya msingi 8
3.2 Matumizi huru ya msitu 8
3.3 Shughuli katika misitu zitakazotozwa ushuru 8
3.4 Mazao yanayohitaji vibali vya uvunaji 8
3.4.1 Utaratibu wa kupata leseni ya uvunaji 8
3.4.2 Mazao mengine ya misitu yatakayokatiwa leseni 9
3.5 Matumizi yasiyoruhusiwa ndani ya msitu 9

4: HAKI NA MANUFAA YA WADAU 11

4.1 Haki 11
4.1.1 Kijiji 11
4.1.2 Halmashauri ya Wilaya 11
4.2 Manufaa 11
4.2.1 Kijiji 11
4.2.2 Halmashauri ya Wilaya 11

5: SHUGHULI ZA KUENDELEZA NA KUTUNZA MSITU 12

5.1 Mikakati ya jumla ya kuendeleza msitu. 12
5.2 Ulinzi wa msitu 12
5.2.1 Ushirikishwaji wa jamii katika ulinzi wa msitu. 12
5.2.2 Walinzi wa doria 12
5.3 Upandaji na utunzaji wa miti 13
5.4 Kusafisha mpaka na barabara za moto 13

6: WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU WA MSITU 14

6.1 Majukumu ya kijiji 14
6.1.1 Serikali ya Kijiji 14
6.1.2 Kamati ya Maliasili 14
6.1.3 Wanakijiji 14
6.2 Halmashauri ya Wilaya 15

7: MAPATO YA MAZAO YA MSITU 16

7.1 Vyanzo vya mapato 16
7.2 Mgawanyo wa Mapato kwa wadau 16
7.3 Matumizi ya mapato 16
7.4.2 Taarifa ya Mapato na Matumizi 17

8: UFUATILIAJI NA TATHIMINI 18
8.1 Ufuatiliaji 18
8.2 Tathimini ya kati na ya mwisho 18
9: MKATABA WA MAKUBALIANO 19
9.1 Madhumuni ya Mkataba wa makubaliano 19
9.2 Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu 19
9.3 Marekebisho ya Mpango 19
9.4 Hatua zitakazochukuliwa dhidi ya ukiukwaji wa utaratibu wa usimamizi 19
10: VIAMBATISHO 21

SURA YA KWANZA

1: UTANGULIZI

Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998 imeweka mazingira mazuri ya wananchi kushiriki kikamilifu katika usimamizi na uendelezaji wa misitu hapa nchini Tanzania. Pia sera hiyo pamoja na mambo mengine inasisitiza ushirikishwaji wa jamii katika kusimamia misitu kwa misingi ya kuchangia katika kuinua kipato ili kuondokana na umaskini. Serikali pia iliandaa Programu ya Taifa ya misitu ya mwaka 2001 ambayo nayo kwa pamoja inasisitiza suala zima la ushirikishwaji wa jamii katika usimamizi wa misitu nchini. Ili kuihakikishia jamii kushiriki katika kutunza misitu ikiwa ni pamoja na vijiji, mashirika yasiyo ya kiserikali na hata watu binafsi kwa misingi ya kuinua kipato serikali ilipitisha sheria mpya namba 14 ya mwaka 2002 ambayo inatoa mtizamo mkubwa katika suala nzima la misitu.

Mpango huu wa usimamizi shirikishi wa msitu wa jamii wa Tawi umerekebishwa na kamati ya maliasili ya kijiji cha Tawi kwa kukishirikiana na serikali ya kijiji pamoja na timu ya wataalamu wawezeshaji wa misitu kutoka Halmashauri ya wilaya ya Rufiji. Mpango huu umetayarishwa kwa kuzingatia taratibu za tamko la Sheria ya Misitu Na. 14 ya 2002. Baada ya kuandaliwa, mpango huu umedhibitishwa na Halmashauri ya kijiji cha Tawi kabla ya kupitishwa na mkutano mkuu wa serikali ya kijiji na baadaye kudhibitishwa na Halmashauri ya wilaya ya Rufiji.

Hatua za kuiandaa jamii katika kutayarisha mpango huu zimefadhiliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Mfuko wa Hifadhi wa Dunia (WWF) kwa ushirikiano na Halmashauri ya wilaya ya Rufiji.

Pamoja na mambo mengine mpango huu umefafanua na kuweka bayana shughuli zote zitakazofanyika katika kipindi cha kutumika kwa mpango zikiwemo shughuli za uboreshaji wa msitu, shughuli za kiuchumi za jamii na taratibu za usimamizi hii ikiwa ni pamoja na mapato, gharama na matumizi yatokanayo na rasilimali za msitu, utunzaji wa kumbukumbu za matukio mbalimbali yatokananayo na msitu na udhibiti wa uhalifu na ufuatiliaji.

Usimamizi wa rasilimali zilizomo msituni utaongozwa na taratibu zilizokubalika kwa kuzingatia sheria ndogo za msitu za kijiji zilizotungwa na kijiji cha Tawi na kuidhinishwa na halmashauri ya wilaya ya Rufiji chini ya sheria ndogo za mazingira za wilaya na sheria mama ya msitu namba 14 ya mwaka 2002.

Mpango huu utatumika kwa kipindi cha miaka mitano (2010 – 2014) kuanzia tarehe ya kupitishwa na utakuwa ukifanyiwa marekebisho pale itakapobidi kwa kusudio la kuuboresha ili kuongeza ufanisi wa usimamizi wa msitu wa Tawi kwa manufaa ya jamii ya kijiji cha Tawi na jamii nzima ya wilaya ya Rufijii na taifa zima kwa ujumla.

1.1 Umiliki wa msitu

Msitu unamilikiwa na serikali ya kijiji cha Tawi. Msitu wa jamii wa Tawi ulitengwa kuwa hifadhi Novemba 2006 chini ya usaidizi wa kitalaamu toka kwa wawezeshaji wa Halimashauri ya wilaya ya Rufiji na wawezeshaji wa Mradi wa Misitu ya Ukanda wa Pwani chini ya WWF.

1.2 Lengo kuu la ya Mpango Shirikishi

Kutunza, kusimamia na kutumia rasilimali za msitu kiuendelevu kwa ajili ya kuhifadhi bioanuwai ya msitu na hatimaye kuboresha na kuendeleza uchumi wa jamii.

1.3 Madhumuni

- Jamii kujenga uwezo endelevu wa kutunza, kusimamia na kutumia rasilimali za msitu.
- Jamii kujijengea uwezo wa kutoa maamuzi juu ya matumizi ya kipato kitokanacho na rasilimali za msitu kwa manufaa ya jamii nzima ya kijiji

1.4 Muda

Mpango huu utatumika kwa kipindi cha miaka mitano (2010 – 2012) kuanzia tarehe ya kupitishwa na utakuwa ukifanyiwa marekebisho pale itakapobidi kwa kusudio la kuuboresha ili kuongeza ufanisi wa usimamizi wa msitu wa Tawi kwa manufaa ya jamii ya kijiji cha Tawi na jamii nzima ya wilaya ya Rufijii na taifa zima kwa ujumla.

SURA YA PILI

2: HISTORIA FUPI YA MPANGO

2.1 Jamii

Kijiji cha Tawi kipo katika kata ya Mbwara, tarafa ya Muhuro, katika Wilaya ya Rufiji.

Kina idadi ya watu wapatao 1,100 katika kaya zipatazo 225, na kina kilomita za mraba zipatazo..... .

Kilisajiliwa mwaka 1974 kwa cheti Na. PW-KJ 306.

Kijiji hiki kinapakana na vijiji vya Nyamwage (Mashariki), Nambunju (kusini), Utunge (Kaskazini), Utete (magharibi) na Mbwara (Kaskazini), vilivyoko katika kata ya Mbwara.

Kijiji hakina Cheti cha ardhi cha kijiji , lakini mipango ya matumizi bora imeshafanyika na taratibu zipo mbioni kupata cheti hicho. Mipaka ya kijiji imewekwa mawe ya alama.

Vitongoji vya kijiji vinavyotambulika ni: Kiboko, Mkukiki na Gege. Kati ya hivyo vitongoji vya Gege na Mkukiki viko karibu na msitu wa jamii.

2.2 Maelezo kuhusu Msitu

2.2.1 Mahali ulipo Msitu na ukubwa wake

Msitu wa hifadhi wa Tawi upo katika ardhi tambarare ya ukanda wa Pwani wa bahari ya Hindi. Msitu upo umbali wa kilometa 56 kusini mwa mji wa Ikwiriri katika wilaya ya Rufiji kupitia Kijiji Nyamwage na Mbwara.

Msitu wa hifadhi wa Tawi upo katika kijiji cha Tawi ukiwa umezungukwa na msitu wa matajiwazi wa kijiji. Upande wa kasikazini msitu umepakana na bonde la Mbulibuli, Magharibi ni eneo huria la kijiji cha Tawi mpakani na wilaya ya Rufiji, Kusini ni msitu wa Malenge mpakani na wilaya ya Kilwa na Mashariki umepakana na bonde la Mtepeke ambalo limepakana na msitu wa taifa wa Kiwengoma na vijiji vya Nambunju na Mbwara. Eneo la msitu ni hekta za mraba 2,787.

2.2.2 Uoto wa asili na Mazingira.

Sehemu kubwa ya msitu wa Tawi ina uoto wa miti ya aina ya miombo iliyochanyika na vichaka vilivyojitokeza baada ya uvunaji mkubwa uliofanyika kati ya miaka ya 1985 mpaka 1990. Hivi sasa bado ipo miti mikubwa ambayo inaweza kuvunwa na mingi ya miti hii ni ile ambayo hapo awali haikuwa na soko. Miti aina mninga, mkongo, msekeseke, mvule, mpingo na mkuruti ambayo soko lake ni kubwa imevunwa kwa kiwango kikubwa na hivi sasa imeadimika ndani ya msitu. Machipukizi na miti michanga inayojitokeza inahitaji kutunzwa ili iweze kukua katika maeneo yake ya asili.

2.2.3 Rasilimali za misitu.

Jamii za miti

Msitu wa Tawi ni msitu wenye rasilimali nyingi ikiwa ni pamoja na aina mbali mbali ya miti inayotumika kwa shughuli za mahitaji ya jamii (Kiambatisho Na 1). Matumizi makubwa ya miti hii ni pamoja na mbao na magogo kwa ajili ya biashara. Miti mingine ni kwa ajili ya matunda, dawa, kuni na mijengo. Pia msitu huu una wanyama wa aina mbalimbali ambao wanategemewa na jamii (kiambatisho na 3).

Utambuzi wa rasilimali msituni

Uchambuzi wa matumizi ya miti iliyopo msituni umeonyesha kuwa ipo miti ipatayo 20 ambayo matumizi yake ni makubwa katika biashara ya magogo na mbao. Kwa ujumla kijiji cha Tawi hupata ajira ya ukataji wa magogo kutokana na leseni zinazotolewa na serikali. Upasuaji wa mbao hufanyika kwa maficho na wananchi wenyewe.

Kwa mpango huu kijiji sasa kitasimamia msitu wa Tawi na uvunaji utazingatia upatikanaji wa miti iliyoorodheshwa katika Mpango wa uvunaji. Kwa kutumia utambuzi wa majina ya miti iliyopo katika msitu wa Tawi, miti iliyoorodheshwaMpango wa uvunaji ndiyo ambayo inatumika kwa biashara ya magogo na mbao. Kwa zoezi la kutambua miti lililofanyika na wananchi wakati wa kutengeneza mpango huu imeonyesha kuwa miti aina ya *mninga, mkongo, mvule, msekeseke, mkuruit, mkangazi, mkunungu, mpangapanga, muhama, Mpangati, Mgama, Mmangagwaru* imevunwa kwa kipindi kirefu na hivi sasa imekuwa adimu kupatikana msituni.

Kiwango cha matumizi

Kwa uzoefu wa wananchi na mwelekeo wa soko la biashara ya magogo na mbao hivi sasa miti iliyopewa 3 ndiyo ambayo hapo awali haikupendelewa kuvunwa na wateja hivi sasa kijiji kinaweza kutumia mpango endelevu wa uvunaji ulioandaliwa na kuvuna miti hii katika msitu wao kwa viwango vya uvunaji vilivyoonyeshwa. Uvunaji uzingatie miti iliyokomaa yenye mzunguko kuanzia sentimeta 100 (raundi 5) katika usawa wa kifua. Idadi ya miti aina mbali mbali ipatayo 8 kwa kila hekta moja inaweza kuvunwa mara moja kila baada ya miaka kumi. Uuzaji wa mazao ya msitu utafuata bei za serikali (kiambatisho Na 4). Mazao mengine yataendelea kupatikana katika msitu uliopo kijijini kwa vile msitu uliotengwa upo mbali na maeneo ya makazi ya watu.

Msitu huu utagawanywa katika maeneo kumi ya uvunaji kwa kuzingatia ukubwa na mtawanyiko wa miti. Kila eneo la uvunaji litavunwa mara moja kwa mzunguko wa miaka kumi.

Aina ya miti ilyopo msituni, upatikanaji na matumizi yake

Aina za miti iliyopo msitu na upatikanaji wake umeonyeshwa kwenye Mpango wa Uvunaji wa Msitu wa Tawi.

Mazao yasiyotimbao

Jamii ya kijiji cha Tawi inategemea msitu wao kwa shughuli mbali mbali hii ikiwa ni pamoja na mazao timbao kama vile magogo, mbao na mijengo (kiambatisho na 1). Mazao yasiyo timbao yanayotegemewa na jamii ni kama vile Ming'oko, Uyonga, Matunda, asali, dawa kutoka miti mbali mbali, Angai, Ndeng'ende, Makurume, Ulanga Nyasi, Miyaa na Ukindu kwa usuzi. Pia nyama kutokana na wanyama pori ambao hutumika kama chakula (kiambatisho na 3).

Ukusanyaji wa takwimu za mazao ya misitu

Matokeo ya Tathmini Shirikishi ya Rasilimali za misitu kwa kijiji chaTawi. yameonyeshwa katika Mpango wa Uvunaji wa Msitu wa Tawi

2.2.4 Wanyama pori na jamii za mimea

Msitu huu una wanyama wa aina mbalimbali ambao wanategemewa na jamii (kiambatisho na 3)

2.2.5Maeneo madogo ya Usimamizi.

Msitu huu una kanda moja ya usimamizi kiikolojia ambayo itatumika kama kanda ya matumizi. Kutokana na ukubwa wa msitu huu ikiwa ni pamoja na wingi wa miti iliyomo ndani, msitu huu utagawanywa katika maeneo kumi ya uvunaji ambapo kila eneo litavunwa mara moja katika

kipindi cha mzunguko wa miaka kumi. Kwa kufuata utaratibu huu wa uvunaji maeneo na miti iliyoathirika inaweza kurudia hali yake ya zamani kwani hakutakuwepo na uvurugaji wa uoto wa asili hasa miti michanga kwa kipindi cha miaka kumi ya mzunguko.

Pia msitu uko katika mcakato wa Uthibitishaji wa Msitu (Forest Cetification), hivyo matumizi yataangaliwa kwa ukaribu zaidi na ushauri wa kitaalamu kwa mahitaji ya soko la nje. Kijiji kinatarajia kuungiza msitu katika cheti cha Uthibitishaji wa Misitu kinachomilikiwa na Mradi wa Mpingo (Mpingo Conservation Project (MCP))

2.3 Matumizi ya Msitu

2.3.1 Mambo ya asili & Haki za kijadi

Elezea kama kuna mila na haki za kijadi zinzotumika msituni.(matumizi ya jadi)

2.3.2 Historia ya nyuma

Msitu wa Tawi upo katika kanda ya misitu ya Pwani katika wilaya ya Rufiji ndani ya kijiji cha Tawi. Hapo awali mmiliki wa msitu huu alikuwa serikali kuu chini ya usimamizi wa halmashauri ya wilaya ya Rufiji. Matumizi ya msitu huu yalikuwa huria ukiwa unavunwa na wananchi kutoka nje na ndani ya kijiji cha Tawi na vibali vya uvunaji vilitolewa bila ya kuwepo na ufuatiliaji wa kutosha.

2.3.3 Matumizi ya sasa

Kijiji cha Tawi kiliomba kusimamia msitu huu baada ya kuona uharibifu uliokuwa unaendelea wa uvunaji huria. Taratibu za upimaji zimefanyika, uwekaji wa alama za mpaka kwa kuchimba mashimo yenye mwelekeo wa mpaka wa msitu umefanyika kuzunguka msitu wote ikiwa ni pamoja na uchoraji ramani mwaka 1999. Msitu huu ulitangazwa rasimi kuwa msitu wa hifadhi wa kijiji cha Tawi mwaka 2002.

SURA YA TATU

3: MWONGOZO WA MATUMIZI YA MAZAO YA MISITU.

Vipengele katika sura hii vinaweka bayana taratibu za kuingia msituni na za matumizi ya mazao ya msitu. Wale ambao hawatafuata taratibu hizi watapigwa faini.

3.1 Matumizi ya msingi

- Wanakijiji cha Tawi ndio wanaoruhusiwa kuingia katika msitu wa jamii kwa shughuli mbali mbali za usimamizi kufuatana na taratibu zilizokubalika.
- Mtaalamu yo yote wa msitu anaweza kuingia msituni kwa shughuli yoyote bila ya kuchukua kitu ndani ili mradi ametoa taarifa kabla ya kuingia kwa serikali ya kijiji.
- Watu wengine kutoka nje ya kijiji cha Tawi wataruhusiwa kuingia ndani ya msitu wa Tawi kwa vibali maalumu.
- Mazao ambayo ni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kama vile dawa za tiba, matunda, miyaa, ukindu, uyoga, fito, nyasi, mboga, angai, mingoko, makurume, mijengo na kuni yanaruhusiwa kuchukuliwa msituni na wanavijiji bila ya malipo ila kwa kupata kibali cha kufanya hivyo.
- Mazao yote ya msitu ambayo ni kwa ajili ya biashara yatachukuliwa msituni kwa kulipia ushuru na kutakuwepo na utaratibu maalumu wa kusafirisha nje ya kijiji.

3.2 Matumizi huru ya msitu

Matumizi huru kwa wanakijiji wa Tawi yatakuwa kwa ajili ya mazao yasiyotimbao kama vile uyoga, matundapori, mbogamwitu, kuni, nyasi, madawa ya asili na kutundika mizinga katika msitu wa kijiji, vyote hivyo vitapatiwa kibali maalum cha bure toka mjumbe wa kamati ya maliasili kwa kushirikiana na mwenyekiti wa kitongoji.

Wasio wakazi wa kijiji cha Tawi wanaweza pia kuomba kibali toka kamati ya maliasili ya kijiji kutumia mazao yaliyotajwa hapo juu toka msitu wa jamii. Kamati ya maliasili itakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mazao ya msitu ya bure yanatumiwa kiendelevu na hayamalizwi toka msitu wa jamii.

3.3 Shughuli katika misitu zitakazotozwa ushuru

Mazao yote ya uvunaji kama uvunaji wa magogo, mbao na mawe. Bei za uvunaji wa mazao haya zitafuata taratibu zilizowekwa na serikali kwa kutumia kanuni ya misitu ya mwaka 2004 chini ya sheria ya misitu namba 14 ya mwaka 2002 (Kiambatisho Na 4)

- Utalii na mafunzo kwa wageni kutoka nje ya wilaya ya Rufiji
- Uvunaji wa wanyama pori na ndege utafuata taratibu za kupata kibali kupitia Idrara ya Wanyama pori.

3.4 Mazao yanayohitaji vibali vya uvunaji

3.4.1 Utaratibu wa kupata leseni ya uvunaji

Utaratibu huu utahusisha miti ya jamii zifuatazo:

- Mbao
- Magogo
- Makuti kwa ajili ya ujenzi

Ili kupata leseni/kibali cha uvunaji utaratibu ufuatao utafuatwa:

- Mtu yeyote atakayetaka kuvuna mazao ya misitu katika msitu wa jamii itambidi kuandika barua ya maombi kwa serikali ya kijiji ikionyesha aina na kiasi gani cha mazao ya misitu anayotarajia kuvuna toka msitu wa kijiji.
- Serikali ya kijiji ikiwemo kamati ya maliasili itajadili maombi na kuyapitisha kama itaridhia kama ilivyobainishwa katika mpango kazi.
- Afisa Misitu akishirikiana na kamati ya maliasili atafanya makisio ya gharama za mazao ya misitu yaliyoombwa.
- Mwombaji atalipa gharama za kibali/leseni kwa Kamati ya Maliasili na atapatiwa stakabadhi halali.
- Mwombaji atapeleka stakabadhi ya malipo kwa Afisa Misitu wa Wilaya, ambaye atampatia leseni ya kuingia msituni na kuvuna zao lililokubaliwa.
- Mwombaji atarudi tena kijijini kupeleka leseni yake kwa Kamati ya Maliasili, kamati itamwonyesha eneo la kuvuna mazao ya misitu anayoyahitaji.
- Baada ya kuvuna, magogo na visiki yatagongwa alama ya kijiji (nyundo ya kijiji).
- Mwisho mwombaji lazima apate kibali cha kusafirishia toka kwa Afisa Misitu Wilaya ili aweze kusafirsha mazao yake bila usumbufu nje ya Wilaya.

3.4.2 Mazao mengine ya misitu yatakayokatiwa leseni

- Wanyama pori watalipiwa ushuru sawa na sheria ndogo ya kijiji husika ila ushuru huo usizidi viwango vya sheria mama.
- Mazao yote yaliyotajwa katika kifungu cha 3.1 (iv) pamoja na mazao mengine yasiyotimbao yatakayokubalika na kupitishwa na mkutano mkuu wa kijiji. Pia mkutano mkuu wa kijiji unaweza kuagiza baadhi ya mazao yaliyotajwa katika kifungu cha 3.1 (iv) kulipiwa na kuwekewa bei.
- Miti kwa ujenzi au ukarabati kwa huduma za jamii kijijini.
- Utundikaji wa mizinga ndani ya msitu
- Utafiti kwa wadau wote na mafunzo kwa wakazi wa wilaya ya Rufiji
- Kuchunga mifugo ndani ya msitu

3.5 Matumizi yasiyoruhusiwa ndani ya msitu

- Kuvuna miti iliyoadimu ikiwa ni pamoja na miti iliyoathiriwa kwa kiwango kikubwa katika uvunaji holela uliokuwa umefanyika hapo awali kama vile Mninga, Mkongo, Mpingo, mvule na mkangazi.
- Kuanzisha kilimo ndani ya msitu
- Kuweka makazi ndani ya msitu
- Kurina asali mahali popote msituni ikiwa siyo kwenye mizinga iliyotundikwa msituni.
- Kutega wanyama au ndege
- Kuchimba madini ndani ya msitu

Kuingia msituni

Mtu atakayeingia msituni kwa kibali cha kulipia ni lazima awe na mwelekezaji kutoka kijijini.
Taratibu za kulipia vibali/ushuru ili kuingia na kuchukua rasilimali msituni zitabadilika kufuatana na mabadiliko ya kiuchumi.

3.6 Taratibu za utoaji taarifa



3.6.1 Taarifa za kawaida

Mfumo wa usimamizi utakaotumika ni kama ulivyoorodheshwa kwenye jedwali namba 2 na utoaji wa taarifa za kawaida utafuata utaratibu hapo chini. Taarifa za kawaida zifuate utaratibu wa utoaji taarifa uliopo kama ulivyoonyeshwa

Jedwali Na 2: Mfumo wa kutoaji taarifa za kawaida

3.6.2 Taarifa za dharura

Masuala yote ya dharura kama vile matukio ya moto taarifa zitolewe kwa kiongozi yo yote aliyepo karibu kwa utekelezaji na baadaye taarifa zikiendelea kutolewa kwa kufuata taratibu za ngazi husika.

3.6.3 Taarifa zenye utata

Mara nyingi taarifa zenye utata ni zile zinazowahusisha viongozi waliopo madarakani katika ngazi ya kijiji. Pale palipo na taarifa za uharibifu wa aina yo yote katika msitu na mmoja kati ya ngazi za uongozi anahusika ukipeleka swala hilo katika ngazi hiyo ni wazi halitapewa uzito unaositahili hivyo kama ni lazima taarifa zitolewe katika ngazi za juu zaidi.

SURA YA NNE

4: HAKI NA MANUFAA YA WADAU

4.1 Haki

4.1.1 Kijiji

- Kumiliki na kutunza msitu wa Kijiji cha Tawi
- Kutumia rasilimali ndogondogo bila mashariti magumu kama ilivyobainishwa katika mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu.
- Kukusanya na kutumia ushuru na mapato mengine yatokanayo na mazao ya misitu katika shughuli za maendeleo ya jamii.
- Kufanya maamuzi juu ya usimamizi na matumizi ya msitu.
- Kutumia msitu kuboresha hali za maisha ya jamii.
- Kusimamia maliasili zote kwenye msitu wa jamii.

4.1.2 Halmashauri ya Wilaya

- Kupokea taarifa za nusu mwaka juu ya utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa msitu.
- Kukagua vitabu vya mapato na matumizi na kuchukua hatua zinazotakiwa kama italazimu.
- Kuchukua msitu kama kijiji kitashindwa kuusimamia ipasavyo
- Kushauri maswala yote ya utunzaji wa misitu
- Kusaidia vitendea kazi,ulinzi, usafiri na utaalamu

4.2 Manufaa

4.2.1 Kijiji

- Kutumia miti na mbao kwa ajili ya ujenzi na ukarabaji wa huduma za jamii kijijini.
- Mapato yatokanayo na faini na ushuru wa mazao ya misitu.
- Kupata mafunzo ya kitaalam katika masuala mbalimbali.

4.2.2 Halmashauri ya Wilaya

- Kupungua kwa gharama za usimamizi wa misitu.
- Kuboresha uhifadhi wa misitu.
- Kupungua kwa migogoro na migongano inayohusiana na matumizi ya misitu kati ya Halmashauri ya Wilaya na jamii.

SURA YA TANO

5: SHUGHULI ZA KUENDELEZA NA KUTUNZA MSITU

Kutokana na msitu kuwa uoto wa aina moja, msitu mzima utakuwa na eneo moja la usimamizi. Mikakati ya jumla ya kutunza na kuendeleza msitu pamoja na rasilimali zake imewekwa bayana. Mambo yatakayoangaliwa ni upandaji wa miti na utunzaji wa machipukizi dhidi ya moto, ulinzi wa msitu, kinga na uthibiti wa moto pamoja na mpango wa matumizi endelevu wa mazao ya msitu.

5.1 Mikakati ya jumla ya kuendeleza msitu.

Katika kuendeleza msitu, mikakati ya jumla itakayofanyika ndani ya msitu ni kama ifuatavyo:-

Ndani ya msitu

- Kudhibiti matukio ya moto.
- Kuthibiti uvunaji holela wa mazao ya misitu
- Kudhibiti uwindaji haramu katika maeneo yote ya msitu.
- Kudhibiti urinaji wa asali kwa kutumia moto.
- Kuweka mabango ya aina mbalimbali yenye ujumbe wa hifadhi.
- Kuanzisha mashamba ya nyuki ndani ya msitu.
- Kufyeka na kupanda miti katika mpaka wa msitu ili uweze kutambulika kwa urahisi

Nje ya msitu

- Kuanzisha matumizi bora ya ardhi
- Kuhimiza uhifadhi vyanzo vya maji
- Kuhimiza uanzishaji wa mashamba ya nyuki na ufugaji bora wa wanyama kama mbuzi, ng'ombe na kuku.
- Kuhimiza uhifadhi na utunzaji wa misitu ya asili katika maeneo ya jamii ikiwa ni pamoja na kupanda miti.
- Kuelimisha wananchi juu ya taratibu za utumiaji moto katika kuandaa mashamba na uwekaji wa barabara za kuzuia moto kuzunguka maeneo ya misitu.
- Kuhamasisha jamii juu ya uanzishwaji wa vikundi vya kiuchumi na kimaendeleo.
- Kuimarisha njia za ukusanyaji mapato yatokanayo na mazao ya misitu kijijini.

5.2 Ulinzi wa msitu

Usimamizi wa msitu wa jamii utakuwa chini ya serikali ya kijiji na utatunzwa na wanajamii. Jamii nzima ya kijiji cha Tawi watahusika katika ulinzi wa msitu kila mmoja katika nafasi yake kwa kutoa taarifa ya aina yoyote au kuwajibika wenyewe pale watakapoona uharibifu.

5.2.1 Ushirikishwaji wa jamii katika ulinzi wa msitu.

Msitu utalindwa na jamii kuzingatia mipaka yake, kila mtu atatoa taarifa kwa uongozi wa kijiji au kamati ya maliasili au kikosi cha doria pale anapoona uharibifu katika msitu. Kamati ya maliasili itaratibu na kusimamia shughuli za doria.

5.2.2 Walinzi wa doria

Suala la ulinzi wa msitu wa Tawi ni jukumu la jamii nzima ya wanavijiji wote. Kila mwanakijiji atahusika katika ulinzi wa msitu kila mmoja katika nafasi yake kwa kutoa taarifa ya aina yoyote au kuwajibika wenyewe pale watakapoona uharibifu.

Kamati ya doria ikisaidiana na kamati ya maliasili na serikali ya kijiji watafanya doria mara 4 kwa mwezi na Kamati mara 2 kwa mwezi ili kudhibiti uhalifu msituni. Kamati ya doria ndiyo mhusika mkuu katika kufuatilia na kutoa taarifa kwa kamati ya maliasili.

5.3 Upandaji na utunzaji wa miti

Upandaji na utunzaji wa miti utahitajika kama kutakuwa na upungufu wa miti ya jamii fulani kutokana na uvunaji kwa siku za nyuma na uchomaji moto ovyo. Kijiji cha Tawi kimechagua baadhi ya jamii za miti kuwa inafaa kwa mpango wa upandaji kwa sababu ya tathmini imeonyesha kuwa jamii hizo zipo kwa idadi ndogo. Jamii hizi za miti ni Mninga, Msufipori, Mtondo, Mpangapanga na Mkongo. Jamii za miti inayotumika kwa ujenzi ambayo inahitaji upandaji ni Mkolamakoa, Msagawi, Mjongoo, Msenjele, Mkonge, Mkiu, Mtatu, Mkulyungu and Mkalambati.

5.4 Kusafisha mpaka na barabara za moto

Mpaka wa msitu umechimbwa mashimo yenye kuonyesha mwelekeo wa mipaka kwa msitu wote. Hakuna mawe ya mpaka ambayo yamewekwa kwa msitu mzima. Mawe ya mpaka wa msitu pamoja ufyekaji na upandaji wa miti ya mpaka ndilo hitaji kubwa la msitu wa Tawi.

SURA YA SITA

6: WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU WA MSITU

Msitu wa kijiji cha **Error! Reference source not found.** una wadau wafuatao; (Serikali ya Kijiji, Halimashauri ya Wilaya ya Rufiji, serikali na wadau wa (WWF). Majukumu ya kila mdau yameelezewa kama ifuatavyo:

6.1 Majukumu ya kijiji

Katika kuimarisha usimamizi shirikishi wa msitu, kijiji kimekubaliana kuwa na kamati mbili za utekelezaji. Kamati hizo ni pamoja na kamati ya doria (kikosi cha ulinzi) itakayokuwa na mjumbe mmoja kutoka katika kila kitongoji jumla wajumbe 5. Endapo idadi ya watu watano haitatimia vitongoji jirani na msitu vipewe nafasi za zaidi ya kutoa wajumbe wa doria. Halmashauri ya kijiji itapendekeza majina na kupitishwa na mkutano mkuu wa kijiji.

Kamati ya pili ni kamati ya maliasili ya kijiji ambayo ina wajumbe 12 waliochaguliwa na mkutano mkuu wa kijiji. Kuwepo kwao madarakani kutakwenda sambamba na uongozi wa serikali ya kijiji cha Tawi.

6.1.1 Serikali ya Kijiji

- Kutekeleza majukumu yote yaliyobainishwa kwenye makubaliano.
- Kupokea na kuidhinisha utekelezaji wa makubaliano yote yaliyofikiwa na halmashauri ya kijiji juu ya kuendeleza msitu
- Halmashauri ya Kijiji kupendekeza wajumbe wa kamati ya maliasili na doria

6.1.2 Kamati ya Maliasili

Kamati ya Maliasili ina majukumu yafuatayo:

- Kuratibu shughuli zote za kikosi cha doria.
- Kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo
- Kuelimisha jamii juu ya matumizi endelevu ya rasilimali za misitu
- Kupokea, kujadili na kutolea mapendekezo wateja wanaomba uvunaji wa mazao ya msitu kwa halmashauri ya kijiji.
- Kutenga maeneo ya ya uvunaji na idadi ya wavunaji kwa kila eneo husika
- Kutoa vibali baada ya kukubalika kutoka katika serikali ya kijiji.
- Kufuatilia vibali vilivyotolewa na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika msitu.
- Kupokea taarifa za kikosi cha doria, kuandaa taarifa na kuziwasilisha kwa serikali ya kijiji.
- Kuandika na kutunza kumbukumbu za taarifa mbalimbali za shughuli za msitu
- Kutoa mapendekezo ya bajeti ya utekelezaji wa mpango shirikishi kwa halmashauri ya kijiji.
- Kukusanya mapato yote yatokanayo na mazao/huduma za msitu.
- Kuandaa programu na malengo ya kazi zitakazofanyika kila mwaka na kusimamia utekelezaji wake.
- Kupokea na kutekeleza mabadiliko yote ya usimamizi kutoka ngazi za juya.

6.1.3 Wanakijiji

- Kuzuia uharibifu wowote utakaojitokeza katika msitu kama vile uchomaji moto na uvunaji holela wa mazao ya misitu.

- Kutoa taarifa ya uharibifu wa aina yeyote utakaofanyika ndani ya msitu kwa Kamati ya Maliasili na serikali ya Kijiji.
- Kushiriki katika shughuli zote za kuboresha msitu.
- Kupitia na kuidhinisha inapofaa sheria ndogo zilizopendekezwa na Kamati ya Maliasili.
- Kushiriki katika doria za kulinda msitu mara kwa mara.

6.2 Halmashauri ya Wilaya

- Kuhimiza uanzishaji wa vikundi vya maendeleo.
- Kutoa wataalamu watakaosaidia jamii katika kutekeleza mpango shirikishi
- Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa shughuli zote za msitu.
- Kuhamasisha wananchi juu ya matumizi bora ya ardhi pamoja na maliasili zake.
- Kusimamia na kushauri juu ya utekelezaji wa sera na sheria za misitu
- Kupokea na kuidhinisha mapendekezo ya sheria ndogo za msitu
- Kutafuta masoko ya kueleweka ya mazao yatokanayo na Misitu.
- Kufuatilia na kukagua mapato na matumizi ya fedha za kijiji zitokanazo na maliasili ikiwa ni pamoja na kuimarisha njia za ukusanyiaji mapato.
- Kupokea na kutolea ushauri taarifa za ufuatiliaji ili kuboresha dhana nzima ya usimamizi shirikishi

Idara ya Misitu Na Nyuki

- Kusaidia kuratibu utafutaji wa masoko ya mazao na bidhaa zitokanazo na misitu
- Kutunga na kusimamia sera na sheria za msitu kulingana na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii

Mkaguzi wa Mahesabu

Kwa kuwa ukaguzi wa hesabu vijijini hufanywa na Halmashauri ya Wilaya, vivyo hivyo ukaguzi wa fedha za kamati za maliasili vijijini zitafanywa na Halmashauri ya Wilaya na taarifa yake kutolewa kwa halmashauri ya kijiji. Pia mkaguzi atahusika kutoa mafunzo kwa mweka hazina juu ya taratibu sahihi za kuweka mahesabu ya mapato na matumizi ya fedha za maliasili.

6.3 Serikali kuu na wadau

- Kutoa watalaam washauri pale wanapohitajika.
- Kutoa miongozo mbalimbali inayohusu usimamizi misitu.
- Kusaidia jamii katika kutekeleza majukumu mbali mbali yaliyoainishwa ndani ya mpango shirikishi.
- Kusaidia jamii kutafuta masoko ya mazao ya misitu na mazao mengine na kuweza kubaini njia rahisi za kufikia masoko hayo

SURA YA SABA

7: MAPATO YA MAZAO YA MSITU

7.1 Vyanzo vya mapato

- Huduma za msitu (kiambatisho Na 5) na ushuru wa mazao
- Ada za mafunzo, tafiti mbalimbali na utalii
- Mauzo ya mazao ya msitu
- Faini za wahalifu
- Misaada na tunuku ya zawadi kutoka njee na ndani ya nchi.

7.2 Mgawanyo wa Mapato kwa wadau

Kipaumbele cha matumizi ya mapato yatokanayo na msitu yataelekezwa katika shughuli za kuendeleza msitu kwa kuzingatia shughuli zilizopangwa katika mpango wa kazi wa mwaka. Kijiji kitatenga fedha za kutosha za kuendesha shughuli za maliasili ili kuhakikisha kuwa mapato endelevu yanakuwepo yatakayosaidia kuchangia katika maendeleo ya kijiji.

Pakiwepo na dharura inayohitaji matumizi ya fedha kama vile moto uongozi wa kijiji utaidhinisha matumizi na kutoa taarifa hiyo katika mkutano mkuu wa kijiji.

7.3 Matumizi ya mapato

- Ununuzi wa vifaa vya kazi kama vile
  (i) viatu vya doria (ii) baiskeli (iii) kalamu (iv) panga (v) sare (vi) makoti ya mvua
- Ununuzi wa vitabu vya kumbukumbu kama vile (i) Kumbukumbu za vikao (ii) doria (iii) uhalifu (iv) mapato na matumizi (v) hati ya malipo (vi) stakabadhi ya fedha (vii) vibali (viii) kitabu cha wageni na (ix) fomu za taarifa ya ufuatiliaji
- Gharama za usafiri na posho kwa kamati na wajumbe wengine kwenye mikutano na shughuli za kikazi
- Uendelezaji wa shughuli za hifadhi ya msitu kama vile kufyekea na kupanda miti mpakani na katika maeneo ya kijiji.
- Motisha au posho kwa kikosi cha doria
- Utengenezaji wa vipeperushi kwa ajili ya kutangaza msitu.
- Kulipia gharama za uendeshaji wa kesi zinazohusiana msitu wa Nambunju mahakamani.

Matumizi ya kijiji

Matumizi ya kijiji ni pamoja na shughuli mbalimbali za maendeleo kama vile ujenzi wa shule, barabara, zahanati nk.

Mgawanyo wa mapato yatokanayo mazao/huduma za misitu

Mgawanyo wa mapato yatokanayo na mazao/huduma za misitu utakuwa kati ya serikali ya kijiji cha Tawi na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji. Mgawanyo huu utazingatia nani mwenye majukumu makubwa zaidi katika kusimamia, kutunza na kuendeleza msitu.

Mgawo wa mapato yote ni kama ifuatavyo

- Kijiji kitapata asilimia sabini (70%)
- Halmashuri ya Wilaya itapata asilimia thelathini (30%)

Mapato ya kijiji yatatumika kwa shughuli za maendeleo ya kijiji (asilimia 50) na katika kuboresha shughuli za msitu kwa kuzingatia shughuli zilizopangwa katika mpango wa kazi wa mwaka (asilimia 50).

7.4 **Usimamizi wa Fedha**

Fedha zote zitatunzwa benki isipokuwa kwa fedha chache kwa ajili ya matumizi madogodogo. Pesa ndogondogo haitakiwi kuzidi shilingi 50,000/=. Kutakuwa na akaunti benki itakayofunguliwa kwa jina la Akaunti ya Msitu wa Jamii. Kutakuwa na watia sahihi wanne; Afisa Mtendaji wa Kijiji (A), Mjumbe mmoja wa Kamati ya Mipango ya Kijiji (A), Mwenyekiti (B) na mweka Hazina (B) wa Kamati ya Maliasili ya kijiji. Mtia sahihi mmoja wa A na mmoja wa B watahitajika kuchukua pesa toka benki.

7.4.1 Vitabu muhimu vya kutunza kumbukumbu vinavyotakiwa

Mweka Hazina wa Kamati ya Maliasili atakuwa na jukumu la kutunza vitabu vya kumbukumbu. Vitabu vitakaguliwa na;

- Kamati ya fedha na mipango ya serikali ya kijiji.
- Mkaguzi wa ndani wa Halmashauri ya Wilaya.

Vitabu vitakavyokaguliwa ni;

- Jalada la kumbukumbu/muhitasari wa vikao.
- Kitabu cha kumbukumbu za doria.
- Kitabu cha kumbukumbu za uhalifu.
- Vitabu vya vibali na leseni.
- Kitabu cha stakabadhi za malipo yote yaliyofanyika kulingana na mpango kazi huu.
- Kitabu cha matumizi madogo madogo kwa ajili ya kumbukumbu za matumizi ya pesa ambazo hazikuwekwa katika akaunti ya benki.

7.4.2 Taarifa ya Mapato na Matumizi

Ukaguzi wa mahesabu ya fedha za maliasili utafanyika na mkaguzi wa fedha wa halmashauri ya wilaya. Baada ya taarifa hiyo kupitiwa na hamashauri ya kijiji itawasilishwa kwenye mkutano mkuu wa kijiji. Kabla ya mkutano mkuu wa kijiji tarifa hiyo ya fedha itakuwa imewekwa katika mabango kwenye ofisi ya kijiji siku tano kabla ya mkutano ili wananchi waisome na kuweza kuchangia hoja zao

7.4.3Uwajibikaji

Mwanakamati au mwanakijiji yeyote atakayepatikana na kosa la kutumia vibaya fedha za msitu atawajibishwa na serikali ya kijiji au atashitakiwa katika Baraza la usuluishi la kata au Mahakama ya mwanzo. Mjumbe yeyote wa Kamati ya Maliasili atakayepatikana na kosa lazima ajiuzulu haraka na uchaguzi mpya utafanyika kumchagua mjumbe mwingine kuziba pengo hilo.

SURA YA NANE

8: UFUATILIAJI NA TATHIMINI

8.1 Ufuatiliaji

Kijiji kupitia kamati ya maliasili kitafuatilia shughuli zote za kazi zilizopangwa kwa kipindi chote cha miaka miwili ya utekelezaji wa mpango. Ufuatiliaji huu utahakikisha kuwa shughuli hizo zimefanyika na kukidhi malengo yaliyowekwa katika kusimamia, kuendeleza na kutumia msitu.

Ufuatiliaji utafanyika kila mwaka na kutolewa taarifa ambayo itawezesha kupima kiwango cha utekelezji ili kuweza kufanya mabadiliko ya lazima kwa msingi wa kuweza kufikia lengo kabla ya kipindi cha utekelezaji kumalizika. Ufuatiliaji katika mwaka wa pili ambao ni mwaka wa mwisho wa utekeleji mpango kabla haujafanyiwa marekebisho ndio utakaotoa mwelekeo namna malengo yalivyofikiwa.

Shughuli zitakazofuatiliwa

- Matukio ya moto (Tahadhari zilizochukuliwa)
- Taarifa za doria na utekelezaji wake
- Shughuli za uendelezaji msitu.
- Taratibu za uvunaji na viwango vya uvunaji
- Taratibu za vibali, ukusanyiaji mapato na matumizi ya fedha za msitu
- Ukusanyaji na uwekaji wa kumbukumbu za takwimu za msitu.
- Taratibu za utoaji taarifa na utekelezaji wake.
- Ujengaji wa uwezo kwa jamii na taratibu za usimamizi wa msitu
- Utumiaji wa sheria ndogo za vijiji za kusimamia msitu
- Uundaji wa vikundi vya kiuchumi.

Wahusika katika ufuatiliaji

Ufuatiliaji wa doria litakuwa jukumu la kikosi cha doria kwa taratibu za kuingia msituni mara moja kila wiki na kujaza fomu ya doria (Kiambatisho Na 6). Kamanda wa doria anakabidhi fomu iliyojazwa kwa kamati ya maliasili mara baada ya doria kumalizika.

Kamati ya Maliasili pia itafanya ufuatiliaji kwa kutembelea sehemu zote za msitu mara nne kwa mwezi na kuhakikisha kwamba taarifa za kamati ya doria ni sahihi na shughuli zilizokuwa zimepangwa zimetekelezwa kama ilivyokuwa imekusudiwa. Kamati ya maliasili itaandaa taarifa ya kila mwezi (kiambatisho Na 7) na kuipeleka kwa afisa misitu wa wilaya na nakala kwenye serikali ya kijiji.

Uongozi wa kijiji utafuatilia kwa kupata taarifa kutoka katika kamati ya Maliasili kwa kuhudhuria mojawapo ya vikao vya kamati na kupata taarifa za utekelezaji wa shughuli walizokuwa na wasiwasi nazo, kuongea na kamati kwa kuitisha kikao cha wanakamati na kwa kutembelea msituni. Mwenyekiti na Mtendaji wa serikali ya kijiji watatembelea msitu mara moja kwa mwezi kuona hali ya msitu.

8.2 Tathimini ya kati na ya mwisho

Tathimini ya shughuli mbali mbali zilizofanywa kwenye msitu itafanyika kila mwisho wa mwaka na afisa misitu wilaya akiwa na kamati ya maliasili. Tathimini hii ya kila mwaka italenga shughuli zote za kazi kama zitakavyokuwa zikiainishwa kwenye mpango wa kazi wa kila mwaka. Kupitia tathimini hii mafanikio ya shughuli zilizofanyika kwenye msitu yanaweza kupimwa na kutoa mwelekeo wa shughuli zitakazofuata.

SURA YA TISA

9: MKATABA WA MAKUBALIANO

MAKUBALIANO YA USIMAMIZI SHIRIKISHI WA MSITU WA JAMII KIJIJI CHA TAWI KATI YA SERIKALI YA KIJIJI CHA TAWI NA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI

9.1 Madhumuni ya Mkataba wa makubaliano

Makubaliano haya yamefikiwa kati ya wadu watajwa hapo juu ili eneo la msitu wa Tawi liweze kusimamiwa na wanakijiji cha Tawi kwa ajili ya kusimamia na kuboresha utunzaji wa msitu huu ili hatimaye uweze kutumika kiuendelevu kwa muda mrefu katika kukidhi mahitaji ya jamii ya kijiji cha Tawi.

Majukumu na haki kwa kila upande

Sehemu hii ya mkataba wa makubaliano inaweka bayana haki na faida za kila upande zitakazotambuliwa na pande zote mbili. Majukumu ya Serikali ya kijiji na Halmashauri ya wilaya yameainishwa katika sura ya tano ya mpango huu.

.

9.2 Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu

Mkataba huu wa makubaliano unasisitiza kuwa jamii ya kijiji cha Tawi haina budi kutunza, kusimamia na kuendeleza msitu wao kufuatana na mpango huu wa usimamizi

.

9.3 Marekebisho ya Mpango

Katika kipindi cha utekelezaji wa mpango huu endapo jamii ya kijiji cha Tawi itafanya marekebisho ya jambo lo lote katika mpango huu haina budi marekebisho hayo yataarifiwe kwa afisa misitu wa wilaya naye atatoa maoni yake juu ya marekebisho hayo. Marekebisho hayo yakikubalika yataambatishwa kwenye mpango huu na kutiwa sahihi. Afisa misitu wa wilaya anaweza kutia sahihi kwa niaba ya Mkurugenzi mtendaji wa wilaya.

Marekebisho ya mpango huu yatafanyika baada ya kipindi cha miaka miwili ya utekelezaji ambapo mapungufu yote yatakayojitokeza yatashughulikiwa.

9.4 Hatua zitakazochukuliwa dhidi ya ukiukwaji wa utaratibu wa usimamizi

Endapo kijiji kitashindwa kuutunza na kuusimamia msitu wa Tawi, Halmashauri ya wilaya ina madaraka kamili ya kuchukua msitu huu na kuwa chini ya mamlaka yake mpaka hapo kijiji kitakapoonyesha tena uwezo wa kuutunza.

9.5 WAWEKA SAINI

Mpango huu wa usimamizi wa msitu wa kijiji cha Tawi umesainiwa na:

1. **Sahihi za Mpango wa Usimamizi wa Misitu za Oktoba 2006 zinaheshimiwa. Na pia**

2. **Masahihisho yaliyofanyika Septemba 2010 yamesainiwa na Afisa Misitu wa Wilaya**

   ……..

   Jina:……

   Tarehe:……

10: VIAMBATISHO

Na

1 Aina ya miti na matumizi yake

2 Wanyama waliopo Msituni

3 Mchanganuo wa daraja na bei za mazao ya msitu

4 Mpango wa kazi mwaka 2006/08

5 Huduma na viwango vya malipo

6 Fomu ya doria

7 Fomu ya taarifa ya kila mwezi

Kiambatisho Na 1: Ramani ya Msitu wa Tawi



Kiambatisho Na2: Aina ya miti ilyopo msituni, upatikanaji na matumizi yake

Na	Kiswahili	**Upatikanaji**	**Jina la kienyeji**	**Matumizi**
	Mchekela	**3**		Mbao, magogo, kuni
	Mfichu	3	Mfulu	Matunda, kuni
	Mgama	1		Magogo & mbao
	Miombo	2		Magogo
	Mkangazi	1		Magogo & mbao
	Mkarati	3		Magogo
	Mkenge	3	Mtanga	Mbao & magogo
	Mkongo	1		Mbao & magogo
	Mkuchimbi	2		Mbao na matunda
	Mkuruti	**1**		Magogo, kuni, mbao
	Mkwaju	2		Matunda & kuni
	Mmangagwani	1		Magogo
	Mnandondo	2		Mbao & kuni
	Mnangu	3		Mbao na magogo
	Mtete	3		Kuni na mijengo
	Mnepa	3		Magogo
	Mninga	1		Mbao, kuni
	Mngagati	**3**		Magogo
	Mpangapanga	**1**		Magogo & kuni
	Mpangati	**1**		Magogo
	Mpingo	1		Magogo
	Mpilipili	1	Mpilipili	Mbao na Matunda
	Mpromosia	2	Mmangangwa	Magogo & mbao
	Msekeseke	1		Magogo, mbao mkaa
	Msoro	3		Mbao, mkaa
	Msufi			Mbao
	Mtanga	2		Mbao
	Mtasi	2		Majengo,nguzo,pau
	Mtete	3		Mijengo, Pau, kuni
	Mtondoro	2		Mbao, Magogo, Kuni
	Mtopetope	2		Matunda
	Mtumiba	2		Matunda
	Muuya	2		Mbao
	Mvule	1		Magogo & mbao
	Mwani	2		Mbao , magogo
	Mzambarau		Mzambarau	Matunda
	Nyamakwengwe	3		Magogo
	Usofu			Matunda
	Vitolo			Matunda

Kielelezo: 1 = Adimu kupatikana 2 = Upatikanaji wake ni wastani

3 = Inapatikana msituni

Kiambatisho 3: Aina ya wanyama – msitu wa Tawi

Na	Majina ya Aina ya wanyama Msituni	
	Kiswahili	**Kienyeji**
1.	Simba	Iimba
2.	Tembo	Ndembo
3.	Chui	Obe
4.	Nyati/Mbogo	Njate
5.	Nyumbu	
6.	Nondoli	
7.	Swala	
8.	Mbalapi	
9.	Mbutuka	
10.	Sungura	
11.	Mbawala	
12.	Mbala/Paa	Mbali
13.	Pundamilia	
14.	Nguruwe pori	Ngwe
15.	Nyani	Nkumburo
16.	Ngiri	Ndimini
17.	Ngedere	Kitumbi
18.	Kima	Njei
19	Funo	
20	Mbalape	
21	Tandala	

Kiambatisho Na 4

Mchanganuo wa miti ya asili kwa madaraja na bei zake. Ushuru unalipwa kwa magogo ya mita ya ujazo yaliyopimwa yakiwa na maganda yake.

Daraja	**Jina la kiswahili/Kienyeji**	**Jina la kitaalamu**	**Bei TAS**
I	-E.A.Blackwood, mipingo, mugembe	Dalbergia melanoxylon	70,000.00
	- Ebonony, mgiriti, msindi, Mnumbuli, mkulvi	Diospros ebenum/mespiliformis	
	- Mperamwitu, mguruwe, Mkwaya	Combretum stuhlmanii	
	- Mvule, mkongola, Iroko	Milicia excelsa	
	- Mninga, mkula, mngubi, mtumbati, mtoni, mkurungu Mninga maji	Perocarpus all spp.	
	- Mfimbo, mkweo, mkanta	Beilschimeidia kweo	
	- Msandali, Sandal wood	Osyris santallum	
	- Pangapanga, mpande	Millettia stulhmani	
	- Muhuhu, mhugwe, mkarambti	Brachylaena hiillensis	
	- Loliondo, mchiyo,mshisho, brown, olive, mzira, E.A.olive, mtagala, mwalambo, mkimba-kubwa	Olea all spp	
	- Paurosa, kasanda, msekeseke	Swartzial madagasearensis	
	- Mkangazi, mwamiovu	Khaya authotheca	
II	- Adina, mgusia, mdogowe, mgwena	Breanadia salicina	60,000.00
	- Afzelia, mkora, mkongo,mafu, mfuru, mbambakofi	Afzelia quanzensia	
	- Mtambara. mtambaa	Cephalosphaera usambarensis	
	- Mrie, mongo, muwondo, mbokoboko, mkalikali	Entandophragma all spp.	
	- Mtua, mkunguni, mtongoti	Garagaropsis angolensis	
	- Hagenia, mwanga, luziluzi	Hagenia abyssinica	
	- Pencil cedar, mtarakwa, mwangati	Juniperus procera	
III	- Mtalawanda	Markhamia all. spp	50,000.00
	- Mtalawanda	Newtonia all spp.	
	- Mshashita, mdadauka, mkufi, mpunga, Newtonia	Newrobial all spp.	
	- Camphorwood, mkulo, mseri, muheti, maasi	Ocotea usamberensis	
	- Mikoko	Mangrove all spp.	
	- Mwanzi, mlanzi	Oxytenanthera abyssinica	
	- Mabula, mule, msabula, msawula	Parinari curatellifolio	
	- Podo, mse, msisimu, mtokosi	Podocarpus all spp.	
	- Mzambarau, mvengi	Syzygium cummnii	
	- Mfudo	Vitex Kenyansis	
	- Bird plum, mgandu, Mnago,mkuni, okoo, nyabumbu	Bercha,ia discolor	
	- Mbanga, muwanga, afromosia	Percorpsis angolensis	
	- Muhulu, Mgoma,	Minusopsis kumei	
	- Mberimberi, mfu, mulembelembe	Chysophyllum spp.	
	- Bekea, Mkarati, Magando, Msangala	Burkea Africana	
	- Mtundu, Myombo, Mkuti	Brachystegia all spp.	
	- Muba, Mvuva. Mtondo, Mtondoro, mwangati, msima, mtundu, mgombo, muwa, mpanate	Julbernadia all spp.	
	- Balphia, Mkuruti, Mkuranga	Balphia kirkii	
	- Mfurangi, Mtanga, Mdurasi, Mvimbafura, mukingu, Omurera, Mshai, Mboromo, Mhenge	Albizial all spp.	
	- Bangawanga, Mjeringwe	Erythrophleum guineense	
Dara	**Jina la kiswahili/Kienyeji**	**Jina la kitaalamu**	**Bei TAS**

ja			
III	- Misanda, mwavi, mbaraka, mkarati, mloka	Spirostachys africana	50,000.00
	- Msaraka, muharaka, mwaraka	Ambygonocarpus angolensis	
	- Mhozya, mluze, mgude, mfune, mkweanyani, moza, mkweranyani, mkwelangedere, mbalamwezi, mguwa, mperamusim ,palamusi, mwingirangidengi, mkungulanga	Sterculia all spp.	
	- Mkambala, mtambara, muhama	Acacianigrescens	
	- E.A. Mulberry, kumbu, mkuzafunta	Morrus lactea	
	- Filcalhoa, iseta, mkuta	Filcalhoa laurifolia	
	- Pillar wood, ndiri, msadora	Casipourea Malosana	
	- Nkoba, (Uganga Walnut), msau, mukusu, Kilimanjaro mahogany	Lovoa brown/swynnertonii	
	- Codyla, mroma, mgwata	Cordly africana	
	- Nusizi,muhumula, musika	Maesopsis eminii	
	- Mukumari,mringaringa,msingati	Cordia africana	
	- Erkebegia. Msisi, tiwe, msaimbi, ol mikumo	Erkergia ruppeliana	
IV	- Mburumo, dimu, mkalikisumu, lemonwood	Xymalos monospora	40,000.00
	- Mifuka, msisi, lisega	Fauzea all spp.	
	- Rapanea, mlimangombe, mwasa, mshiwizo, kidongashawa	Rapanea rhododendroides	
	- Mwindi, mnepa, mparu, mgofu, makwenzi	Pteleopsis myrtifolia	
	- Msufi – mwitu, mfume	Bombax rhodognaphalon	
	- Amani satin wood, mfarakumbi, mfuakumbi	Faagara amamensis	
V	Aina nyingine yote ya miti ambayo haikuorodheshwa		30,000.00

Angalizo: Mteja anahusika kuvuna mwenyewe

Nguzo kutoka katika msitu wa asili

(a) Kuanzia sentimita 5 ila isizidi sentimita 10 kwenye shina (MOJA) shilingi 200.00
(b) Zaidi ya sentimita 10 ila isizidi sentimita 20 kwenye shina (MOJA) shilingi 250.00

Fito (Miti ya Asili)

Miti yote yenye unene chini ya sentimita 5 (mzigo fito 30) kwa bei ya shilingi 1,500.00

Kuni
Mita ya ujazo shilingi 3,000.00
b) Mzigo mmoja wa kuni kavu (kilo 28) kila siku kwa muda wa mwezi mmoja shililngi 1,000.00

Mkaa
Gunia moja lenye uzito wa kilo 28 Shilingi 600.00

Kiambatisho Na 5: Mpango wa kazi kwa miaka mitano

Mpango wa kazi kuanzia Julai 2010 hadi June 2014

Shughuli ya kazi	Jul09	Aug	Sept	Oct	Nov	Dec	Jan '10-'14	Feb	Mar	Apr	May	Jun	Jul11	Aug	Sep	Oct	Nov	Dec
Kuelimisha jamii juu ya mpango shirikishi																		
Kuweka taratibu za uvunaji na ufuatiliaji																		
Kufanya doria msituni																		
Mafunzo juu ya wajibu na majukumu ya kamati																		
Mafunzo ya utunzaji wa fedha za msitu																		
Mafunzo ya uokotaji mbegu na ukuzaji miche																		
Kufyeka mpaka wa msitu																		
Kutengeneza njia za kuzuia moto ndani ya msitu																		
Kutenga msitu katika eneo la hifadhi na uvunaji																		
Kuweka mabango ya tahadhari ya moto																		
Kutayarisha bustani																		
Kupanda miti mpakani na maeneo ya jamii																		
Mafunzo ya kilimo msitu																		
Kupanda miti kwenye vyanzo vya maji																		
Kuanzisha na kuwezesha vikundi vya kiuchumi																		
Kampaini za moto																		
Mafunzo kwa kikosi cha doria																		
Kutenga mashamba ya Nyuki na kuweka mizinga																		
Kutekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi kijijini																		
Uendeshaji wa miradi midogo midogo																		

Kiambatisho Na 6

Huduma za msitu na viwango vya malipo

Na	Shughuli/Tendo	Raia Mtanzania kwa siku	Wageni kwa siku
1	Utafiti bila kuchukua kitu chochote.	Mtu mmoja shilingi 3,000/=	Mtu mmoja US $ 5
2	Kuingia ndani ya msitu (mtalii)	Mtu mmoja shilingi 1,500/=	Mtu mmoja $ 30
3	Kuweka hema msituni	Hema moja shilingi 1,000/=	Hema moja US $ 20
4	Muongozaji (guard)	Shilingi 1,000/=	Dola US $ 2
5	Kikundi cha Mafunzo	Shilingi 10,000/=	US $ 20

Kiambatisho Na 7
FOMU YA DORIA

Kijiji		Tarehe	
Eneo/Njia		Muda wa kuanzia	
Majina ya Walinzi		Muda wa kumalizia	
1.		4	
2.		5	
3.		6	

Uchukuaji wa rasilimali/Uharibifu/Tishio Msituni
Andika ulichokiona

Na	Aina ya uharibifu	Chanzo cha uharibifu	Idadi/ukumbwa

Viashirio vya kuonekana wanyama aidha kwa kinyesi/nyayo, sauti au kuonekana kwa macho

Na	Jina la mnyama	Idadi Wanyama ulioona	Idadi wanyama/ kinyesi	Idadi ya wanyama - sauti

Maoni mengineyo kuhusiana na hali ya msitu na rasilimali:

Kiambatisho Na 8

Taarifa kutoka Kamati ya maliasili

Kwa: Ofisi ya Ardhi, Maliasili na Mazingira - Rufiji

Nakala: M/kiti kijiji

Msitu wa ----------	**Kijiji:** ----------	**Mwezi na Mwaka:** ----------
Andika jina na cheo cha mjumbe	Wanawake	Wanaume
	1.	1.
	2.	2.
	3.	3.
	4.	4.
	5.	5.
	6.	6.

Mikutano/ Mafunzo	Tarehe	Idadi ya washiriki (KE)	Idadi ya washiriki (ME)	Mada kuu kuhusu Maliasili
Mikutano ya Kamati ya Maliasili				
Mikutano ya Hadhara				
Mafunzo/Warsha				

Idadi ya Vibali, Mapato ya Mazao/ Huduma, Mapato ya Faini na Matumizi

Aina ya Mazao/ Huduma	Idadi ya Vibali	Mapato (Tshs)	Faini	
			Idadi ya faini	
			Mapato ya faini (Tshs)	
			Matumizi ya Maliasili (Tshs)	
Jumla ya idadi ya vibali na mapato ya mazao/ huduma:	Jumla ya Idadi ya vibali	Jumla ya Mapato ya mazao/ huduma	Matumizi ya Kijiji (Tshs)	
			Jumla ya Matumizi	Tshs

Idadi ya doria zilizofanyika……

Mambo yaliyoibuliwa----------

Maoni Mengine:

Tarehe:	Tarehe:	Tarehe:
……..……	…….	……
Sahihi	Sahihi	Sahihi
Katibu wa Kamati Maliasili	Mwenyekiti Kamati ya Maliasili	Mwenyekiti wa Kijiji